SEHEMU YA TATU

MIKUTANO NA VIKAO

Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya

18.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya utaanza tarehe na saa ile ambayo Bunge jipya limeitishwa na Rais kukutana.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hizi kuhusu kuanza na kufungwa kwa vikao vya Bunge, Mkutano wa Kwanza wa Bunge utaendelea kukutana kwa muda wowote ambao utahitajiwa ili kutekeleza na kukamilisha shughuli zote za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya.

Shughuli za Mkutano wa Kwanza

19.-(1) Shughuli za Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya zitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Uchaguzi wa Spika;
(b) Kiapo cha Uaminifu kwa Wabunge wote;
(c) Hoja ya kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu;
(d) Uchaguzi wa Naibu Spika;
(e) Ufunguzi rasmi wa Bunge Jipya utakaofanywa na Rais;
(f) Hoja ya kujadili hotuba ya Rais;

(2) Mwanzoni mwa Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, Katibu atasoma Tangazo la Rais la kuliita Bunge Jipya kukutana na baada ya hapo atasoma Dua.

(3) Mara tu baada ya Dua kusomwa, Bunge litaingia katika shughuli ya uchaguzi wa Spika. Kwanza; Katibu atamwomba Mbunge asiyekuwa Waziri, au rngombea wa nafasi hiyo ya Spika, kutoka miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa Wabunge kwa mfululizo kwa muda mrefu zaidi kuliko Wabunge wengine, awe Mwenyekiti wa Bunge kwa madhumuni ya kuongoza shughuli za uchaguzi wa Spika. Kisha atagawa karatasi za kura kwa Wabunge, na

uchaguzi wa Spika utafanywa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 7.

(4) Baada ya shughuli za uchaguzi wa Spika kumalizika, Mwenyekiti atasitisha Shughuli za Bunge hadi wakati atakaoutaja, ambapo Bunge litarudia kwa ajili ya Spika mteule kuapishwa.

(5) Bunge litakaporudia, Mwenyekiti atamwita Spika mteule ajongee ili aapishwe. Spika mteule atajongea kwenye Meza ya Kiapo. Katibu atasimama mahali pake na, akielekeza maneno yake kwa Spika mteule, atasoma maelezo yafuatayo:-

> Mheshimiwa ..... ninayo heshima kukuarifu kwamba, Wabunge wa Bunge hili Tukufu, katika kutekeleza masharti ya lbara ya 84(l) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wamekuchagua wewe Mheshimiwa ..... uwe Spika wa Bunge hili. Kwa hiyo basi, kutokana na na kuchaguliwa kwako, sasa nakuita wewe Mheshimiwa ..... Uape Viapo vinavyohusika, kwa mujibu wa msharti ya Kanuni ya 25(2) ya Kanuni za Bunge.

(6) Baada ya Spika kuapishwa, atakalia kiti chake na kutoa shukrani zake; na baada ya hapo ataliahirisha Bunge hadi wakati mwingine atakaoutaja, ambapo shughuli za kuwaapisha Wabunge wote Kiapo cha Uaminifu zitaanza.

(7) Baada ya shughuli za kuwaapisha Wabunge kumalizika, Spika atasoma taarifa ya Rais inayotaja jina la Waziri Mkuu anayependekezwa athibitishwe na Bunge kwa mujibu wa masharti ya lbara ya 51(2) ya Katiba ya Nchi. Baada ya hapo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi huo. Hoja hiyo itajadiliwa na kuamuliwa kama hoja nyingine yoyote.

(8) Baada ya hapo, au wakati mwingine utakaoamuliwa na Spika, Bunge litamchagua Naibu Spika kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 8.

(9) Ikifikia wakati huu, Spika atalitangazia Bunge ni kwa wakati gani

Rais atalifungua Bunge rasmi. Kisha aweza ama kusimamisha shughuli za kikao hadi wakati huo, au kadri itakavyokuwa, kukiahirisha kikao hicho hadi siku na wakati atakaoutaja.

(10) Spika atamkaribisha Rais kulifungua rasmi Bunge jipya. Rais akimaliza hotuba yake ya ufunguzi, Spika atasimamisha kikao kwa muda atakaoutaja ili amsindikize Rais na baada ya hapo itatolewa hoja ya kuahirisha Bunge, hadi siku na wakati utakaotajwa katika hoja hiyo.

Mikutano ya Kawaida ya Bunge

20.-(1) Mikutano yote ya Bunge itafanyika katika Ukumbi wa Bunge Mjini Dodoma.

(2) Bila ya kuathiri masharti yanayofuatia ya Kanuni hii, kila Mkutano, isipokuwa Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, utaanza tarehe itakayowekwa na Bunge lenyewe.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyotangulia ya Kanuni hii, endapo manufaa ya Taifa yatahitaji kuwa Bunge lisikutane tarehe ile iliyowekwa kwa mkutano utakaofuata, bali likutane tarehe ya mbele zaidi au ya nyuma zaidi, basi Spika aweza, baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, kuliita Bunge likutane tarehe hiyo ya mbele zaidi au nyuma zaidi.

(4) Iwapo Bunge litatakiwa kukutana tarehe ya mbele zaidi kuliko ile iliyowekwa na Bunge lenyewe, basi tarehe hiyo mpya haitakuwa mbele zaidi ya siku kumi na nne kutoka tarehe ile iliyowekwa na Bunge lenyewe.

(5) Endapo Wabunge wasiopungua nusu ya idadi ya Wabunge wote watampelekea Spika kwa maandishi ombi lililowekwa saini na Wabunge hao, la kutaka Bunge liitishwe kwa dharura kabla ya tarehe ya kikao kilichopangwa, basi Spika, ataliita Bunge likutane kwa dharura.

Nyakati za Vikao

21.-(l) Kikao cha Kwanza cha kila Mkutano wa Bunge, isipokuwa kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge jipya, kitaanza saa tatu asubuhi, ila tu kama Bunge litaamua vinginevyo.

(2) Vikao vitakavyofuata vitaanza saa tatu asubuhi isipokuwa kama Bunge litaamua vinginevyo. Hoja ya kubadilisha wakati wa kuanza kikao, itatolewa na Waziri na itaamuliwa kama hoja nyingine yoyote. Hoja ya aina hiyo haitahitaji kutolewa taarifa.

(3) Bunge litaendelea kukutana mpaka ifikapo saa saba mchana. Ifikapo saa hiyo, shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika, isipokuwa kama Bunge litaikubali hoja ya kuendelea kukutana kwa muda utakaotajwa, itasimamishwa na Spika bila kuwahoji Wabunge mpaka saa kumi na moja jioni, ambapo shughuli hiyo itaendelea. Isipokuwa kwamba Spika akiona inafaa, aweza kusimamisha Shughuli za Bunge wakati wowote kabla ya saa saba mchana, hadi saa kumi na moja jioni. Kwa siku ambayo Hotuba ya Bajeti itatolewa, shughuli zitasimamishwa hadi saa kumi jioni.

(4) Isipokuwa kama litakuwa limeahirishwa mapema zaidi, Bunge litaendelea kukaa mpaka saa mbili kasorobo usiku, wakati ambapo Spika atasimamisha shughuli na kuliahirisha Bunge bila hoja kutolewa, hadi kesho yake au siku nyingine atakayoitaja. Lakini iwapo hoja ya kuongeza muda wa kikao hicho itatolewa na kukubaliwa, Spika ataliahirisha Bunge wakati muda ulioongezwa utakapomalizika. Hoja yoyote ya kuongeza muda wa kikao haitaomba kuongeza muda unaozidi dakika thelathini. Kama wakati wa kusimamisha shughuli Bunge litakuwa katika Kamati ya Bunge Zima au Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti atasimamisha shughuli za Kamati hiyo na Bunge litarudia.

(5) Iwapo wakati wa kusimamisha shughuli Spika atakuwa anahoji au yupo karibu kuhoji Bunge, basi atachelewesha kusimamisha shughuli mpaka hoja iwe imeamuliwa.

(6) Endapo Spika atakuwa amepokea taarifa ya Mbunge yeyote anayetaka kutoa maelezo yake chini ya fasili ya (9) ya Kanuni hii, basi badala ya yeye kuliahirisha Bunge, Spika atamwita Waziri atakayetoa hoja ya kuahirisha Bunge, ili kutoa nafasi kwa Mbunge huyo aweze kuchangia hoja hiyo kwa kutoa maelezo yake. Lakini itabidi maelezo hayo yawe yameandikwa na kuwasilishwa kwa Spika angalau siku moja kabla hayajatolewa, na Mbunge anayehusika atayasoma kama yalivyoandikwa.

(7) Baada ya kusimamisha shughuli, hakuna shughuli nyingine yoyote itakayofanywa katika kikao hicho isipokuwa kufikiria hoja ambayo itatolewa na Waziri ya kuahirisha Bunge hadi kesho yake au hadi siku nyingine itakayotajwa katika hoja hiyo.

(8) Endapo majadiliano yoyote katika Bunge au katika Kamati ya Bunge Zima yatasimamishwa na Spika kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hii, wakati yatakaporudiwa katika Bunge au katika Kamati, yataendelezwa kuanzia hapo yaliposimamishwa kana kwamba mjadala uliendelea, na Mbunge yeyote ambaye hotuba yake ilikatizwa na Spika atakuwa na haki ya kuendelea na maelezo yake katika marudio ya mjadala huo. Endapo Mbunge hakuitumia haki yake hiyo, basi atahesabiwa kuwa alikuwa amemaliza hotuba yake.

(9) Bila ya kujali masharti ya Kanuni hii, hoja ya kuahirisha Bunge kwa mujibu wa fasili ya (6), yaweza kutumiwa kama fursa kwa Mbunge yeyote kutoa maelezo yake binafsi, au kutaka ufafanuzi utolewe na Waziri, juu ya jambo lolote lililoko katika madaraka ya Waziri huyo, au kuanzisha mjadala juu ya jambo lolote la dharura kwa idhini ya Spika, isipokuwa jambo ambalo kwa mujibu wa Kanuni ya 50(6), haliwezi kujadiliwa bila hoja maalumu kutolewa kwa ajili hiyo.

(10) Iwapo dakika thelathini zitapita tangu hoja ya kuahirisha Bunge ilipotolewa iamuliwe kabla Bunge halijahojiwa na kuamua hoja hiyo, basi Spika atakatisha mazungunizo yanayoendelea, na papo hapo atalihoji Bunge kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge.

(11) Iwapo shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano hazijamalizika, hoja yoyote ya kuliahirisha Bunge itakuwa ni ya kuliahirisha mpaka kikao kinachofuata ambacho, kama Bunge halikuamua vinginevyo, kitakuwa ni siku itakayofuata, isipokuwa kama itakuwa ni siku ya Jumamosi, Jumapili au siku ya mapumziko.

(12) Ikitokea dharura yoyote, Spika anaweza kusimamisha shughuli za Bunge bila kuwahoji Wabunge.

Kufunga Mkutano

22.-(l) Kila Mkutano wa Bunge utafungwa kwa kuliahirisha Bunge hadi Mkutano utakaofuata.

(2) Endapo shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Mkutano huo zimemalizika, hoja ya kuahirisha Bunge itataja siku na saa ambapo Mkutano utakaofuata utaanza.